Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto

IDARA YA USTAWI WA JAMII NA WAZEE

# MPANGO WA PENSHENI JAMII ZANZIBAR (ZUPS)

# Yaliyomo.

- Utangulizi
- Malengo ya kuanzishwa kwa Pensheni Jamii Zanzibar
- Vigezo vya kusajiliwa katika Mpango wa Pensheni Jamii
- Muundo wa Pensheni Jamii
- Hali ya utekelezaji wa Mpango kwa sasa
- Idadi ya walengwa (Takwimu)
- Mafanikio
- Changamoto
- Hitimisho na mipango ya baadae

# Utangulizi

- Mpango wa Pensheni Jamii ni matokeo ya utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014,
- Sera hiyo imeeleza wazi mkakati wa kuanzisha Pensheni Jamii kwa wazee kutokana na changamoto zinazowakabili wazee ikiwa ni pamoja na ukosefu wa usalama wa kipato
- Mpango huu ni kwa ajili ya wazee wa Zanzibar wenye miaka 70 na kuendelea.
- Mchakato wake ulianza mwaka 2015 kwa zoezi la kuwasajili wazee wote wa Unguja na Pemba ambao wametimiza umri wa miaka 70 na kuendelea kwa kuwapitia nyumba hadi nyumba.

# Inaendelea……

❖Programu hii inaendeshwa kupitia sheria ya wazee namba 2 ya mwaka 2020 pamoja na Muongozo wa Utekelezaji wa Pensheni Jamii.

❖Tarehe 15/04/2016 Pensheni Jamii ilizinduliwa rasmi na ilianza kwa kuwalipa wazee elfu ishirini taslimu.

❖ Jumla ya wazee 21,263 waliweza kulipwa pensheni,Unguja wazee 12,722 na Pemba wazee 8,541.

**Malengo ya Pensheni Jamii Zanzibar**

- Kuweza kutekeleza kwa vitendo Sera ya Hifadhi ya Jamii ya Zanzibar ya mwaka 2014
- Kuwawezesha wazee kuwa na uhakika wa usalama wa kipato cha kila mwezi

# Vigezo vya kusajiliwa katika Mpango

Mzee anaweza kuomba pensheni jamii iwapo ametimiza vigezo vifuatavyo:

- Ni mzee mwenye umri wa miaka 70 au zaidi,
- Ni mkaazi wa Zanzibar; au
- Amekuwa akiishi Zanzibar kwa zaidi ya miaka 10 mfululizo baada ya kufikia umri wa miaka 18.

# Muundo wa Pencheni Jamii



# Utekelezaji wa Mpango wa Pensheni Jamii kwa sasa

Mpango wa Pensheni Jamii Zanzibar unatekelezwa na kufadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Utekelezaji huo unafanyika katika maeneo matatu muhimu yafuatao:-

- Ofisi za Sheha : Kujaza fomu za maombi ya wazee wa miaka 70
- Ofisi za Wakuu wa Wilaya: kupokea na kuhakiki fomu za maombi ya wazee wa Pensheni kutoka  ofisi za masheha na kuzipeleka kitengo cha Pensheni Jamii
- Kitengo cha Pensheni Jamii : kuratibu na kusimamia zoezi la pensheni jamiii ikiwa ni pamoja na kuyakubali maombi yote  ya wazee kutoka Ofisi za Wilaya

# Idadi ya wazee wanaopokea pensheni

| OKTOBA,2021 | IDADI | W'KE | W'UME |
|---|---|---|---|
| UNGUJA | 17607 | 10321 | 7286 |
| PEMBA | 11545 | 6695 | 4850 |
| JUMLA | 29152 | 17016 | 12136 |

# Mafanikio

- Kuweza kutekeleza zoezi la pensheni Unguja na Pemba
- Kuwa na usafiri wa uhakika katika kuendesha zoezi la Pensheni Jamii. Kitengo kina gari mbili (basi moja na pick up moja).
- Kuwepo kwa mfumo wa mpya wa kisasa wa kuhifadhia taarifa za wazee pamoja na malipo.
- Kuweko kwa sheria Namba.2 ya mwaka 2020 ya wazee inayoutambulisha rasmi kisheria Mpango wa Pensheni Jamii

# Changamoto

- Eneo dogo la ofisi kulingana na ukubwa wa shughuli za kitengo zinazofanywa
- Uhaba wa wafanyakazi katika kitengo cha Pensheni
- Kukosekana kwa mafunzo ya kujengewa uwezo kwa watendaji wa Kitengo cha Pensheni Jamii.

# MPANGO WA BAADAE

- Kutayarisha kanuni za uendeshaji wa mpango wa pensheni jamii
- Kuengeza watendaji wa Kitengo cha Pensheni Jamii ili kukamilisha majukumu ya kitengo kwa ufanisi zaidi na kwa wakati unaohitajika.

# AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA